# Afya na Mazingira

## Kitabu cha Mwanafunzi

### Darasa la Pili



Taasisi ya Elimu Tanzania

*Mali ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Hakiuzwi*

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

# Afya na Mazingira

## Kitabu cha Mwanafunzi
## Darasa la Pili



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA ELIMU, SAYANSI
NA TEKNOLOJIA

*Cheti cha Ithibati*

Na. 564

Jina la Chapisho: Afya na Mazingira Kitabu cha Mwanafunzi Darasa la Pili

Mchapishaji: Taasisi ya Elimu Tanzania

Mwandishi: Taasisi ya Elimu Tanzania

ISBN: 978-9987-09-314-4

Kitabu hiki kimeidhinishwa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia tarehe 12 Julai, 2021 kuwa Kitabu cha Kiada kwa ajili ya Mwanafunzi wa Darasa la Pili katika ngazi ya elimu ya Msingi nchini Tanzania kulingana na Muhtasari wa Mwaka 2015.

Dkt. Lyabwene M. Mtahabwa
Kamishna wa Elimu

**Taasisi ya Elimu Tanzania**

FOR ONLINE USE ONLY

Afya na Mazingira STD 2 _ 22 June 2021.indd 1 7/23/21 4:07 PM

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

© Taasisi ya Elimu Tanzania, 2018

Toleo la Kwanza 2018

Toleo la Pili 2021

ISBN 978 - 9987 - 09 - 314 - 4

Taasisi ya Elimu Tanzania
S.L.P. 35094
Dar es Salaam
Simu +255 735 041 170 / 735 041 168
Baruapepe director.general@tie.go.tz
Tovuti www.tie.go.tz

Haki zote zimehifadhiwa. Hairuhusiwi kunakili, kurudufu, kupiga chapa, kutafsiri wala kukitoa kitabu hiki kwa namna yoyote ile bila idhini ya maandishi ya Taasisi ya Elimu Tanzania.

FOR ONLINE USE ONLY



Afya na Mazingira STD 2 _ 22 June 2021.indd 2 7/23/21 4:07 PM

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

# Yaliyomo

**Utangulizi**......iv
**Shukurani**......v

**Sura ya Kwanza**
Mwili wa binadamu......1

**Sura ya Pili**
Njia mbalimbali za kujikinga na magonjwa......10

**Sura ya Tatu**
Mazingira yetu ......39

**Sura ya Nne**
Huduma ya kwanza ......51

**Sura ya Tano**
Viumbe hai katika mazingira......59

FOR ONLINE USE ONLY



Afya na Mazingira STD 2 _ 22 June 2021.indd 3 7/23/21 4:07 PM

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

# Utangulizi

Mazingira safi huleta afya bora. Utunzaji wa afya na mazingira ni muhimu katika maisha. Watoto wenye afya bora hukua vizuri. Kitabu hiki kinasisitiza usafi wa mwili na mavazi. Pia, kinasisitiza kujikinga na magonjwa, usafi wa nyumba na mazingira. Vilevile kinafundisha namna ya kuepuka mazingira hatarishi. Aidha kitabu hiki kinaelezea namna ya kutoa huduma ya kwanza.

Mafundisho haya yatajenga tabia nzuri za afya kwa wanafunzi. Pia yatapunguza matatizo ya kiafya katika maisha. Vilevile, mwanafunzi atajenga stadi za Kusoma, Kuandika na Kuhesabu.

FOR ONLINE USE ONLY



Afya na Mazingira STD 2 _ 22 June 2021.indd 4 7/23/21 4:07 PM

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

# Shukurani

Taasisi ya Elimu Tanzania (TET) inatambua na kuthamini mchango muhimu wa washiriki waliofanikisha uandishi na maandalizi ya kitabu hiki.

TET inatoa shukurani za dhati kwa mchango uliotolewa na wataalamu wote walioshiriki kutayarisha kitabu hiki wakiwemo wachapaji, wasanifu, wahariri, wachoraji na wapiga chapa. Pia, inatoa shukurani kwa shule zote zilizoshiriki katika ujaribishaji wa maudhui na uhariri wa kitabu hiki.

Aidha, Taasisi inatoa shukurani za pekee kwa Shirika la "Global Partnership for Education (GPE)" kupitia Mradi wa Kukuza Stadi za Kusoma, Kuandika na Kuhesabu (KKK) uitwao "Literacy and Numeracy Education Support (LANES)" kwa ufadhili wao uliofanikisha kazi ya kutayarisha na kuchapa kitabu hiki.

Mwisho, Taasisi inatoa shukurani za pekee kwa Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kwa kusimamia kwa ukaribu zoezi zima la uandishi wa kitabu hiki.



**Dkt. Aneth A. Komba**
**Mkurugenzi Mkuu**
**Taasisi ya Elimu Tanzania**

FOR ONLINE USE ONLY



Afya na Mazingira STD 2 _ 22 June 2021.indd 5 7/23/21 4:07 PM


FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

# Sura ya Kwanza

## Mwili wa binadamu



### Katika sura hii utajifunza vipengele hivi

1. Sehemu za nje za mwili wa binadamu.
2. Kazi za sehemu za nje za mwili wa binadamu.
3. Kuchora mwili wa binadamu na kuonesha sehemu zake.

FOR ONLINE USE ONLY




Afya na Mazingira STD 2 _ 22 June 2021.indd 1 7/23/21 4:07 PM

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**Sehemu za nje za mwili wa binadamu**

Angalia picha hii, kisha jibu swali.



Taja sehemu za nje za mwili wa binadamu.

## Kazi ya kufanya

Chora picha ya mwili wa binadamu. Onesha sehemu za nje.

1. Weka karatasi juu ya picha.
2. Tumia penseli kuchora kwa kufuatisha.
3. Ondoa karatasi.
4. Onesha sehemu za nje za mwili wa binadamu.

FOR ONLINE USE ONLY



Afya na Mazingira STD 2 _ 22 June 2021.indd 2 7/23/21 4:07 PM

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Kazi za sehemu za nje za mwili wa binadamu

### Wimbo

Kila sehemu ya mwili ina kazi yake x 2
Haya ni macho kuona ni kazi yake
Huona nini?
Vitu mbalimbali
Hii ni pua kunusa ni kazi yake
Hunusa nini?
Harufu mbalimbali
Haya masikio kusikia ni kazi yake
Husikia nini?
Sauti na milio.

Kila sehemu ya mwili ina kazi yake x 2
Hii mikono kushika ni kazi yake
Hushika nini?
Vitu mbalimbali
Hii miguu kutembea ni kazi yake
Kutembea wapi?
Popote tuendapo
Huu mdomo kula ni kazi yake
Pia kuongea, kazi ya mdomo
Kila sehemu ya mwili ina kazi yake x 2

FOR ONLINE USE ONLY



Afya na Mazingira STD 2 _ 22 June 2021.indd 3 7/23/21 4:07 PM

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

Hizi ni kope
Kuzuia ni kazi yake
Huzuia nini?
Vumbi na takataka
Hii ni ngozi
Kufunika na kuhisi ni kazi yake
Hufunika nini?
Sehemu za mwili
Kuhisi nini?
Joto na baridi

## Zoezi la 1

**Jibu maswali haya.**

1. Oanisha sehemu ya mwili na kazi yake. Chora mistari kama ilivyooneshwa.

**Mfano** Vidole vya miguu – kusaidia kutembea

| Sehemu ya mwili | Kazi yake |
|---|---|
| Vidole vya miguu | Kufunika ngozi ya kichwa |
| Macho | Kutembea |
| Mdomo | Kuzuia vumbi na takataka |
| Masikio | Kusikia |
| Miguu | kusaidia kutembea |
| Mikono | Kuongea na kula |
| Kucha | Kunusa |
| Nywele | Kufunika sehemu laini za vidole |
| Ngozi | Kufunika sehemu za mwili na kuhisi |
| Kope | Kushika vitu |
| Pua | Kuona |

FOR ONLINE USE ONLY



Afya na Mazingira STD 2 _ 22 June 2021.indd 4 7/23/21 4:07 PM

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

2. Ni sehemu zipi za mwili hazijatajwa?
3. Chora na taja sehemu za nje za mwili.


## Kutambua rangi tofauti

Kiungo gani cha mwili kinatumika kuona vitu mbalimbali?

Macho humwezesha binadamu kuona. Mojawapo ya vitu anavyoviona binadamu ni rangi.

### Kazi ya kufanya

Angalia maumbo yafuatayo, kisha jibu maswali yanayofuata.




FOR ONLINE USE ONLY



Afya na Mazingira STD 2 _ 22 June 2021.indd 5
7/23/21 4:08 PM

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**Taja rangi za maumbo uliyoyaona.**

Umbo namba 1 lina rangi ..............................
Umbo namba 2 lina rangi ..............................
Umbo namba 3 lina rangi ..............................
Umbo namba 4 lina rangi ..............................
Umbo namba 5 lina rangi ..............................

## Kutambua milio, sauti za vitu na wanyama mbalimbali

### Kazi ya kufanya

Mwambie rafiki yako aigize sauti na milio mbalimbali.

### Maswali

1. Je, rafiki yako ameigiza mlio au sauti ya nini?
2. Ulitumia kiungo gani kusikiliza mlio au sauti hiyo?

Vitu mbalimbali hutoa milio au sauti. Mfano ndege, kengele, wadudu, wanyama na zeze. Tunasikiliza sauti na milio mbalimbali kwa kutumia masikio.

FOR ONLINE USE ONLY



Afya na Mazingira STD 2 _ 22 June 2021.indd 6 7/23/21 4:08 PM

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Wimbo wa sauti za wanyama mbalimbali

Nyauu, nyauu. Hii sauti ya nini?
Sauti ya paka.
Paka, paka ni rafiki yetu anafukuza panya.

Wu wu. Hii sauti ya nini?
Sauti ya mbwa.
Mbwa, mbwa ni rafiki yetu anatupa ulinzi.

Mee, mee. Hii sauti ya nini?
Sauti ya mbuzi.
Mbuzi, mbuzi ni rafiki yetu anatupa nyama na maziwa.

Moo, moo. Hii sauti ya nini?
Sauti ya ng'ombe.
Ng'ombe, ng'ombe ni rafiki yetu anatupa nyama na maziwa.

### Zoezi la 2

1. Je ni vitu gani ukivitumia vinatoa sauti?
2. Chora vitu vitatu vinavyotoa sauti.
3. Taja majina ya wanyama unayoweza kuigiza sauti zao.

FOR ONLINE USE ONLY



Afya na Mazingira STD 2 _ 22 June 2021.indd 7 7/23/21 4:08 PM

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**Kutambua harufu ya vitu mbalimbali**

Soma habari hii, kisha jibu maswali.

Amani na Upendo wanasoma darasa la pili. Siku moja walipotoka shuleni walikuwa na mazungumzo haya.

**Amani** Hivi ile harufu mbaya darasani huwa inatoka wapi?

**Upendo** Sijui inatoka wapi.

**Amani** Nafikiri kuna baadhi ya wanafunzi hawaogi.

**Upendo** Inawezekana wanaoga ila wanavaa nguo chafu.

**Amani** Kwani nguo chafu husababisha harufu mbaya?

**Upendo** Ndiyo, tena nguo chafu huhifadhi vijidudu vya magonjwa.

**Amani** Lazima tumweleze mwalimu wa afya ili atukague.

Siku iliyofuata Amani alimweleza mwalimu ili wakaguliwe. Mwalimu alikagua mavazi ya kila mwanafunzi. Alipomfikia Papi, harufu mbaya ilizidi. Akamwambia Papi avue viatu. Aligundua soksi za Papi zilikuwa zinatoa harufu mbaya. Akamwambia avue soksi, azipeleke nje na akaoshe miguu. Mwalimu aliwaeleza, ili nguo zisinuke vibaya lazima zifuliwe. Pia zianikwe kwenye jua ili zikauke vizuri. Baada ya masomo Papi alirudi nyumbani. Alipofika nyumbani alivua sare ya shule na kufua. Siku iliyofuata Amani na Upendo hawakuhisi harufu mbaya tena.

FOR ONLINE USE ONLY



Afya na Mazingira STD 2 _ 22 June 2021.indd 8 7/23/21 4:08 PM

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Maswali

1. Katika habari hii umejifunza nini?
2. Mazungumzo yalianzishwa na watu wangapi?
3. Walitumia kiungo gani cha mwili katika mazungumzo?
4. Kiungo gani cha mwili kilitumika kutambua harufu?
5. Andika vitu vitatu vinavyotoa harufu mbaya.
6. Andika vitu vinne vinavyotoa harufu nzuri.

## Zoezi la 3

Tumia maneno yafuatayo kukamilisha sentensi hizi.

**mdomo, Upendo, juani, pua, Papi, mavazi, ngozi, ndani**

1. Sehemu ya mwili iliyotumika kunusa ni ....................
2. Baada ya nguo kufuliwa huanikwa ..........................
3. Soksi za nani zilitoa harufu mbaya? .........................
4. Mwalimu alikagua nini .........................................

FOR ONLINE USE ONLY



Afya na Mazingira STD 2 _ 22 June 2021.indd 9 7/23/21 4:08 PM

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

# Sura ya Pili

## Njia mbalimbali za kujikinga na magonjwa



### Katika sura hii, utajifunza vipengele hivi

1. Usafi wa mwili na mavazi.
2. Usafi wa vyombo vya chakula.
3. Kutunza chakula.
4. Matumizi ya choo.
5. Njia za kujikinga na Virusi vya UKIMWI (VVU).

FOR ONLINE USE ONLY




Afya na Mazingira STD 2 _ 22 June 2021.indd 10 7/23/21 4:08 PM

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Usafi wa mwili na mavazi

Angalia picha zifuatazo, kisha jibu maswali.



1. Picha namba 1 inaonesha mavazi __________
2. Picha namba 2 inaonesha mavazi __________

### Wimbo

Tutaijenga afya kwa kufanya nini? x 2
Tutaijenga afya kwa kuwa wasafi x 2
Tufue nguo zetu na kuzipiga pasi
Tuoge kwa sabuni na kupiga mswaki
Tutaijenga afya kwa kuwa wasafi x 2

Tusafishe masikio kwa kitambaa safi
Tukate nywele na kucha ndefu
Tutaijenga afya kwa kuwa wasafi x 2

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

Usafi wa mwili na mavazi ni muhimu sana. Kwani ni sehemu ya afya bora. Usafi huu husaidia kujikinga na magonjwa.

**Soma habari ifuatayo kisha jibu maswali.**

Matata na Neema wanasoma darasa la pili. Siku moja Matata alikula chakula bila kunawa mikono. Baada ya muda mfupi Matata akaanza kuumwa tumbo. Siku hiyo Matata hakuweza kucheza, maana alikuwa mgonjwa. Matata alipokutana na Neema alimsimulia yaliyompata.

Neema alimuuliza Matata, unakumbuka alivyosema mwalimu? Alisema, tunawe mikono kabla na baada ya kula. Pia alisema tunawe mikono baada ya kutoka chooni. Tena alishauri tusisahau kutumia maji safi na sabuni. Tuoge asubuhi na jioni na kila tunapochafuka. Tunashauriwa kuoga kabla ya kula chakula. Tutumie maji safi, sabuni na dodoki. Mwalimu alisisitiza kusafisha kinywa kila baada ya kula. Alituambia hii husaidia kuondoa mabaki ya chakula.

Matata aliuliza, kwani mabaki ya chakula yanasababisha nini? Neema alijibu yanaleta vijidudu ambavyo husababisha meno kuoza. Pia, mabaki ya chakula husababisha kinywa kunuka. Tulifundishwa kuwa vijidudu pia hujificha kwenye mavazi machafu. Tuliambiwa tufue na tupige nguo pasi kuuwa vijidudu. Matata alisema sitarudia kula chakula bila kunawa mikono. Vilevile, nitasafisha mwili na mavazi kujikinga na magonjwa.

FOR ONLINE USE ONLY



Afya na Mazingira STD 2 _ 22 June 2021.indd 12 7/23/21 4:08 PM

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Maswali

1. Kwa nini Matata aliumwa tumbo?
2. Ni wakati gani tunashauriwa kunawa mikono?
3. Kwa nini tunapiga mswaki?

## Zoezi la 1

Chagua jibu sahihi.

1. Tunaondoa tongotongo kwa ..............
   (kuoga uso / kunawa uso)
2. Wakati unaofaa kuoga ni................. chakula.
   (kabla ya kula / baada ya kula)
3. ............ ili kuondoa mabaki ya chakula.
   (Tunaoga / Tunapiga mswaki)
4. Ni muhimu kunawa ........... baada ya kutoka chooni. (mikono / miguu)
5. ............. husababisha meno kuoza na kinywa kunuka.
   (Vijidudu / Wadudu)

FOR ONLINE USE ONLY


FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Kusafisha masikio

Tunasafisha masikio kwenye mikunjo ya mbele na nyuma. Tunasafisha masikio ili kuua vijidudu vinavyoweza kusababisha magonjwa na kuyaweka yawe safi. Ni hatari kuingiza kitu chochote ndani ya sikio. Sikio likiuma tunashauriwa kwenda hospitalini.

Taja matumizi ya vifaa vinavyotumika kusafishia masikio.


**Vifaa**



## Hatua za kusafisha masikio

1. Loweka kitambaa safi na laini katika maji safi.
2. Paka sabuni kwenye kitambaa kilicholowana.
3. Safisha mikunjo ya mbele ya sikio kwa kitambaa.
4. Safisha sehemu ya nyuma ya sikio kwa kitambaa.
5. Kausha masikio kwa kitambaa laini au taulo safi.
6. Tumia kioo kukagua kama masikio yamekuwa safi.

Vitendo vya kusafisha masikio





Afya na Mazingira STD 2 _ 22 June 2021.indd 14 7/23/21 4:08 PM

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**Kazi ya kufanya**

Safisha masikio kwa kufuata hatua.

**Zoezi la 2**

**Jibu maswali haya.**

1. Andika majina ya vifaa vinavyotumika kusafishia masikio.
2. Taja sehemu za sikio zinazotakiwa kusafishwa.
3. Masikio yakiuma tunashauriwa kufanya nini?
4. Kwa nini ni hatari kuingiza kitu kwenye masikio?

FOR ONLINE USE ONLY

## Usafi wa kucha


Kucha ni sehemu inayofunika ngozi laini ya vidole. Kucha ndefu huhifadhi uchafu. Uchafu huficha vijidudu vya magonjwa mbalimbali.Tukila chakula tukiwa na kucha chafu tutapata magonjwa. Magonjwa hayo ni kipindupindu, kuumwa tumbo na kuharisha. Tunatakiwa kukata kucha zetu ili tuepuke magonjwa. Pia tusichangie vifaa vya kukatia kucha. Kuchangia vifaa husababisha maambukizi ya Virusi vya UKIMWI.





Afya na Mazingira STD 2 _ 22 June 2021.indd 15 7/23/21 4:08 PM


FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

Vifaa vinavyotumika kusafishia kucha



wembe



kikata kucha


sabuni


brashi


mkasi


beseni


taulo

FOR ONLINE USE ONLY

## Namna ya kukata kucha

1. Chukua kifaa safi na salama cha kukatia kucha.
2. Kata kucha ya kidole kimojakimoja.
3. Safisha vifaa ulivyokatia kucha.
4. Safisha kucha za mikono na miguu.
5. Tumia brashi, maji na sabuni kusafishia kucha.
6. Kausha kwa kutumia kitambaa au taulo safi.



Afya na Mazingira STD 2 _ 22 June 2021.indd 16 7/23/21 4:08 PM

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE




Kukata kucha kwa kutumia kikata kucha




Kukata kucha kwa kutumia wembe




Kusafisha mikono kwa maji na sabuni

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

### Kazi ya kufanya

Fuata hatua za kukata kucha. Kata kucha kwa kutumia mojawapo ya vifaa hivi.

1. Wembe
2. Mkasi
3. Kikata kucha

### Zoezi la 3

**Jibu maswali haya.**

4. Taja vifaa vinavyotumika kukatia kucha.
5. Kucha ndefu zinahifadhi nini?
6. Ukichangia vifaa vya kukatia kucha utapata madhara gani?
7. Kwa nini tunakata kucha?

FOR ONLINE USE ONLY


### Kutunza nywele

Angalia picha zifuatazo, kisha jibu maswali.

1



2





Afya na Mazingira STD 2 _ 22 June 2021.indd 18 7/23/21 4:08 PM

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

1. Taja tofauti ya picha namba 1 na 2.
2. Picha gani inakuvutia? Kwa nini?
3. Picha ya mtoto yupi inayofaa kuigwa?

## Kwa nini tunasafisha nywele?

Nywele hushika vumbi kwa urahisi. Yafaa nywele zitunzwe kwa kuoshwa kwa maji safi na sabuni. Pia, zikatwe ili ziwe fupi na zipendeze. Nywele chafu husababisha harufu mbaya ya jasho. Vilevile, huweza kuhifadhi wadudu kama chawa. Chawa hunyonya damu na kusababisha homa kali. Nywele zisafishwe kuepuka magonjwa ya mba na mapunye. Nywele zinafaa kusafishwa kila siku. Pia, tunyoe nywele mara kwa mara. Tuepuke kuchangia vifaa vya kunyolea nywele. Tukichangia vifaa tutapata maambukizi ya magonjwa. Magonjwa hayo ni mba, mapunye na VVU.



Mtoto mwenye mapunye



Afya na Mazingira STD 2 _ 22 June 2021.indd 19 7/23/21 4:08 PM

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Zoezi la 4

**Jibu maswali haya.**

1. Andika faida nne za kunyoa nywele.
2. Ni mdudu gani hupatikana kwenye nywele chafu?
3. Nywele chafu zina madhara gani?
4. Ukichangia vifaa vya kunyoa nywele utapata magonjwa gani?

## Kufua nguo

Soma habari hii, kisha jibu maswali yanayofuata.

Wanafunzi wa darasa la pili walifundishwa kufua nguo. Walielezwa kuwa nguo hufuliwa ili kuondoa uchafu. Uchafu huo husababisha magonjwa ya ngozi. Magonjwa hayo ni kama vile upele, fangasi na miwasho. Nguo safi hudumu na kupendeza. Nguo chafu huhifadhi chawa. Soksi na nguo za ndani zifuliwe kila siku. Tunapofua tutenganishe nguo nyeupe na za rangi. Nguo zifuliwe kwa maji safi na sabuni. Zisuuzwe vizuri kwenye maji safi, kisha zianikwe juani.

## Maswali

1. Kwa nini tunafua nguo?
2. Taja nguo zinazotakiwa kufuliwa kila siku.
3. Tunafua nguo kwa kutumia nini?
4. Nguo chafu husababisha magonjwa gani?


FOR ONLINE USE ONLY




Afya na Mazingira STD 2 _ 22 June 2021.indd 20 7/23/21 4:08 PM

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

Vifaa vya kufulia nguo




beseni la maji




ndoo ya maji




sabuni ya unga



sabuni ya mche



vibanio

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Hatua za kufua nguo

Angalia picha namba 1 hadi 5, kisha fanya zoezi la 5.

1



2



FOR ONLINE USE ONLY



Afya na Mazingira STD 2 _ 22 June 2021.indd 22 7/23/21 4:08 PM

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

3



4



FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

5



## Zoezi la 5

Panga sentensi kwa mtiririko wa matukio katika picha.

1. Suuza nguo kwa maji safi, kisha kamua.
2. Anika nguo kwenye kamba na kuzibana kwa vibanio.
3. Tenganisha nguo za rangi na nyeupe, kisha loweka.
4. Fikicha nguo kuondoa uchafu.
5. Geuza nguo kabla ya kuanika.

FOR ONLINE USE ONLY



Afya na Mazingira STD 2 _ 22 June 2021.indd 24 7/23/21 4:08 PM

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Kazi ya kufanya

1. Fua nguo kwa kufuata hatua za ufuaji.
2. Eleza umejifunza nini kipya katika ufuaji wa nguo ukilinganisha na kabla ya kujifunza.

## Zoezi la 6

**Jibu maswali haya.**


1. Andika sababu tatu za kufua nguo.
2. Taja vifaa vinne vinavyotumika wakati wa kufua nguo.
3. Taja sababu za kutenganisha nguo wakati wa kufua.
4. Kwanini tunatumia sabuni wakati wa kufua nguo?


FOR ONLINE USE ONLY


## Kupiga nguo pasi


Tunapiga nguo pasi ili zinyooke na kuuwa vijidudu. Vijidudu vinaweza kusababisha magonjwa mbalimbali. Magonjwa hayo ni kama vile upele na miwasho. Baada ya kunyoosha nguo, tunazitundika zipate hewa. Hewa huondoa joto la pasi. Joto la pasi husababisha unyevu. Unyevu husababisha nguo kuvunda.

Vifaa vya kupigia nguo pasi


shuka


pasi ya mkaa


pasi ya umeme


meza



Afya na Mazingira STD 2 _ 22 June 2021.indd 25 7/23/21 4:08 PM

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

# Hatua za kupiga nguo pasi

1



2





3





4



FOR ONLINE USE ONLY



Afya na Mazingira STD 2 _ 22 June 2021.indd 26 7/23/21 4:08 PM

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Zoezi la 7

Panga sentensi kwa mtiririko wa matukio katika picha.

1. Mtoto anatundika nguo baada ya kuzinyoosha.
2. Mtoto anaandaa pasi tayari kwa kunyoosha nguo.
3. Mtoto anaandaa meza kwa kutandika shuka.
4. Mtoto anapiga nguo pasi.

## Kazi ya kufanya

Fanya zoezi la kupiga nguo pasi kwa kushirikiana na mwenzako.

## Zoezi la 8

Jaza nafasi zilizoachwa wazi kwa kuchagua maneno haya.

vijidudu, shuka, zisipate unyevu, nadhifu, chafu, kabati.

1. Joto la pasi huua..............
2. Unapopiga nguo pasi unatumia pasi, meza na..........
3. Tunatundika nguo baada ya kupiga pasi ili.........
4. Tunahifadhi nguo iliyonyooshwa kwenye.............

FOR ONLINE USE ONLY




Afya na Mazingira STD 2 _ 22 June 2021.indd 27 7/23/21 4:08 PM

## Usafi wa vyombo vya chakula

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

Vyombo vya chakula ni lazima visafishwe kwa usahihi. Visafishwe kwa kutumia maji safi na sabuni. Vikaushwe kwa kitambaa safi au vianikwe kwenye kichanja. Vyombo visikae kwenye kichanja kwa muda mrefu. Hii husaidia vumbi lisichafue vyombo. Pia husaidia kuvikinga visipate vijidudu vya magonjwa. Vumbi na vijidudu vya magonjwa huvichafua. Vyombo vichafu huvutia wadudu waenezao magonjwa. Nzi, sisimizi na mende hubeba vijidudu vya magonjwa. Magonjwa hayo ni kuharisha, kuumwa tumbo na kipindupindu.


Vifaa vinavyotumika kusafishia vyombo vya chakula



kiosheo



sabuni



beseni

## Hatua za kuosha vyombo vya chakula

1. Andaa vifaa vya kuoshea vyombo.
2. Ondoa mabaki ya chakula kwenye vyombo.



FOR ONLINE USE ONLY




Afya na Mazingira STD 2 _ 22 June 2021.indd 28 7/23/21 4:08 PM

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

3. Tumia sabuni na kiosheo kuosha chombo kimojakimoja.



4. Suuza vyombo kwenye maji safi.
5. Kausha vyombo kwa kutumia kitambaa safi. Kama huna kitambaa anika vyombo kwenye kichanja.



6. Hifadhi vyombo mahali safi ili visichafuke.



FOR ONLINE USE ONLY



Afya na Mazingira STD 2 _ 22 June 2021.indd 29 7/23/21 4:09 PM

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Kazi ya kufanya

Osha vyombo vya chakula kwa kufuata hatua.

### Zoezi la 9

**Jibu maswali haya.**

1. Taja vifaa vinne vinavyotumika kusafishia vyombo vya chakula.
2. Andika majina ya vyombo ulivyowahi kuviosha.
3. Taja sehemu nne za kuhifadhi vyombo vilivyooshwa.
4. Orodhesha magonjwa yanayosababishwa na matumizi ya vyombo vichafu.
5. Taja wadudu wanaovutiwa na vyombo vichafu.
6. Taja sababu mbili za kuosha vyombo vya chakula.


## Kutunza chakula kwa usalama



kawa



ungo



sahani



kifaa cha kuning'inizia chakula

Chakula kinatakiwa kitunzwe kwa usafi na usalama. Chakula kilichotunzwa vizuri hakiharibiwi na wadudu. Mfano wa wadudu wanaoharibu chakula ni mende, nzi na sisimizi. Wadudu wanaoharibu chakula ni mende, nzi na sisimizi. Wadudu hawa hueneza magonjwa kama kuharisha na kipindupindu. Wadudu wanapotua kwenye chakula huacha vijidudu vya magonjwa. Ukila chakula hicho unaweza

FOR ONLINE USE ONLY



Afya na Mazingira STD 2 _ 22 June 2021.indd 30 7/23/21 4:09 PM

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE


kupata magonjwa. Tunatunza chakula ili kiwe salama. Chakula salama uwezesha mwili kuwa na afya bora.

**Zifuatazo ni njia mbalimbali za kutunza chakula**

Kabati la kutunzia chakula.




Jokofu



Kufunika chakula kwa ungo, kawa au sahani.



Kifaa maalumu cha kutunzia chakula kwa kuning'iniza.



FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**Kazi ya kufanya**

1. Andika vifaa vinavyotumika kutunzia chakula.
2. Chora vifaa viwili vinavyotumika kutunzia chakula.

**Zoezi la 10**

**Jibu maswali haya.**

1. Orodhesha magonjwa yanayotokana na kula chakula kisichotunzwa vizuri.
2. Taja wadudu wanaoleta vijidudu vya maradhi kwenye chakula.
3. Taja sababu ya kutunza chakula kwa kukining'iniza.
4. Orodhesha vifaa vinavyotumika kutunza chakula.
5. Taja njia nyingine mbili za kutunza chakula.


## Matumizi sahihi ya choo

Picha ya mtoto yupi anatumia choo kwa usahihi?

1.



2.






FOR ONLINE USE ONLY


Afya na Mazingira STD 2 _ 22 June 2021.indd 32 7/23/21 4:09 PM

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE


Choo ni muhimu kwa matumizi ya binadamu. Choo kitumike kwa usahihi ili kuepuka magonjwa. Kuna aina mbalimbali za vyoo. Mfano, kuna vyoo vya shimo na vya kuvuta. Vyoo vya kuvuta hutiririsha maji yanayoondosha kinyesi.



Choo cha Shimo



Choo cha kuvuta cha kuchuchumaa



Choo cha kuvuta cha kukaa


FOR ONLINE USE ONLY



Afya na Mazingira STD 2 _ 22 June 2021.indd 33 7/23/21 4:09 PM

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Hatua sahihi za matumizi ya choo



1. Funua mfuniko wa shimo la choo kabla hujakitumia.
2. Tumia choo kwa usahihi kwa kulenga shimo.
3. Jisafishe kwa kutumia maji safi baada ya kujisaidia. Vilevile, unaweza kujipangusa kwa kutumia karatasi laini.



Afya na Mazingira STD 2 _ 22 June 2021.indd 34 7/23/21 4:09 PM

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

4. Funika shimo la choo vizuri baada ya kujisaidia.



5. Nawa vizuri mikono kwa maji safi na sabuni.



FOR ONLINE USE ONLY



Afya na Mazingira STD 2 _ 22 June 2021.indd 35 7/23/21 4:09 PM

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Kusafisha choo



Kwa nini tusafishe choo?
Tunasafisha choo kuepuka magonjwa kama kuharisha na kipindupindu. Pia kuondoa harufu mbaya. Choo kisafishwe kwa maji, sabuni na dawa. Baada ya kusafisha choo tunawe mikono. Tutumie maji safi na sabuni.

### Zoezi la 11

**Jibu maswali haya.**

1. Andika vifaa vitatu vinavyotumika kusafisha choo.
2. Taja wadudu wanaopenda kuishi chooni.
3. Taja aina za vyoo unavyovifahamu.
4. Andika magonjwa mawili utakayopata ukitumia choo kichafu.
5. Choo kinachotumika shuleni kwenu ni cha aina gani?
6. Eleza umuhimu wa kujisafisha baada ya kujisaidia.

FOR ONLINE USE ONLY



Afya na Mazingira STD 2 _ 22 June 2021.indd 36 7/23/21 4:09 PM

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Njia za kujikinga na Virusi vya UKIMWI (VVU)

UKIMWI - Ni Upungufu wa Kinga Mwilini.
VVU - ni kifupi cha maneno, Virusi vya UKIMWI.

**Soma habari hii kisha jibu maswali.**

Furaha ni mwalimu katika shule ya Mpakani. Aliwafundisha wanafunzi kujikinga na Virusi vya Ukimwi. Mwanafunzi mmoja alimuuliza mwalimu, utamtambuaje mtu mwenye VVU? Mwalimu alijibu, huwezi kumtambua kwa kumwangalia kwa macho. Ili kumtambua ni lazima apimwe hospitalini.

Mwanafunzi mwingine aliuliza, tunawezaje kupata maambukizi ya VVU? Mwalimu alisema, kwa kuchangia vifaa vyenye ncha kali. Mfano wa vifaa hivyo ni sindano, pini na nyembe. Vilevile vifaa vya usafi kama vitana na miswaki. Pia taulo, dodoki na vifaa vya kunyolea nywele.

Kisha mwalimu alitaja njia za kujikinga na VVU.

1. Epuka kuchangia sindano unapopatiwa matibabu.
2. Epuka kuchangia sindano unapotoga masikio.
3. Funga vidonda wakati wote ili visitoe damu.
4. Epuka kugusa damu ya mtu mwingine.
5. Vaa glovu au mfuko wa plastiki unapomhudumia majeruhi.
6. Epuka kuchangia vifaa kama miswaki, dodoki na vitana.

FOR ONLINE USE ONLY



Afya na Mazingira STD 2 _ 22 June 2021.indd 37 7/23/21 4:09 PM

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Wimbo

VVU ni Virusi vya Ukimwi x 2
UKIMWI ni nini jamani?
UKIMWI ni Upungufu wa Kinga Mwilini jamani x 2
Tusichangie wembe, sindano na mswaki x 2
Tusichangie chanuo, kitana na pini x 2
Tukichangia hivyo tutapata UKIMWI

## Maswali

1. Ili kutambua kuwa umeambukizwa VVU unapaswa kufanya nini?
2. Orodhesha vitu vitano ambavyo vikichangiwa husababisha maambukizi ya VVU.
3. Andika njia tano za kujikinga na VVU.
4. Nini hatari ya kugusa damu ya mwenye VVU?

## Zoezi la 12

Jaza nafasi kwa kuchagua jibu sahihi.

**dodoki, VVU, UKIMWI, kusisitiza, glovu, sindano**

1. ................ ni kifaa cha ncha kali.
2. Kifaa kinachotumika kusugua mwili unapooga ni ..........
3. Kifaa kinachovaliwa mkononi ili kujikinga na maambukizi ya VVU ni .................

FOR ONLINE USE ONLY



Afya na Mazingira STD 2 _ 22 June 2021.indd 38 7/23/21 4:09 PM

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

# Sura ya Tatu

## Mazingira yetu





**Katika sura hii utajifunza vipengele hivi.**

1. Kutumia vifaa mbalimbali kutunza mazingira
2. Kupanda mbegu na miche kwa kuzingatia kanuni
3. Tabia hatarishi katika mazingira
4. Viumbe hatarishi katika mazingira
5. Matumizi ya alama za tahadhari

FOR ONLINE USE ONLY



Afya na Mazingira STD 2 _ 22 June 2021.indd 39 7/23/21 4:09 PM

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Vifaa vya kutunzia mazingira

Mazingira husafishwa kwa kutumia vifaa mbalimbali.

Vifaa vya kusafishia mazingira.



Mazingira ni vitu vyote vinavyotuzunguka kama vile hewa, maji na mimea. Hivyo, inatupasa kusafisha na kutunza mazingira yetu ya nyumbani na shuleni. Mazingira safi huvutia na kupendeza sana. Vilevile, huepusha wadudu na

FOR ONLINE USE ONLY



Afya na Mazingira STD 2 _ 22 June 2021.indd 40 7/23/21 4:09 PM

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

vijidudu vya magonjwa. Hivyo maisha ya viumbe yanahitaji uwepo wa mazingira safi na salama.

**Tazama picha hii kisha jibu maswali.**



**Maswali**

1. Taja vifaa vingine vinavyotumika kusafisha mazingira.
2. Ni wadudu gani wanaopatikana katika mazingira machafu?
3. Baada ya kuokota takataka unapaswa kufanya nini?
4. Mazingira yasiyo safi husababisha madhara gani?
5. Chora picha za vifaa vya usafi wa mazingira.

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Zoezi la 1

Oanisha kifaa na kazi yake. Onesha kwa kuchora mstari.

| Jina la kifaa | Kazi |
|---|---|
| Jembe | huondoa vumbi na uchafu |
| Reki | hutumika kulimia |
| Mkasi mkubwa | hutumika kukusanya nyasi na takataka |
| Fagio | hutumika kuhifadhi takataka kabla ya kuzitupa shimoni |
| Kizoleo | hutumika kukatia maua |
| Pipa | hubebea takataka baada ya kufagia |

## Kazi ya kufanya

1. Safisha darasa kwa kutumia vifaa vya kufanyia usafi.
2. Tumia vifaa vya usafi kusafisha mazingira ya shule.

## Kupanda mbegu na miche kwa kuzingatia kanuni

Miti na maua hupendezesha mazingira na kuyafanya yavutie. Miti husaidia kutunza mazingira yetu. Tunashauriwa kupanda mbegu na miche. Tupande mbegu na miche tupate miti au maua. Kuna kanuni mbalimbali za kupanda mbegu au miche.

Zipo mbegu zinazopandwa moja kwa moja kwenye mashimo. Mfano wa mbegu hizo ni mahindi, maharage na baadhi ya zile za miti. Mbegu nyingine ni lazima kuziotesha ili zitoe miche. Kusia ni kumwaga mbegu kwenye kitalu. Kitalu ni

FOR ONLINE USE ONLY



Afya na Mazingira STD 2 _ 22 June 2021.indd 42 7/23/21 4:09 PM

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

eneo lililoandaliwa ili kuotesha mbegu. Mfano wa mbegu hizo ni nyanya, spinachi na vitunguu.




**Kanuni za upandaji wa mbegu**

1. Andaa kitalu kwa kutifua na kuweka mbolea.
2. Mwagilia kitalu ili udongo uwe na unyevu.
3. Sambaza mbegu kwenye kitalu.
4. Funika kitalu kwa nyasi kavu ili kuhifadhi unyevu.
5. Mwagilia kila siku hadi miche itokeze.



Afya na Mazingira STD 2 _ 22 June 2021.indd 43 7/23/21 4:09 PM

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE



6. Ondoa nyasi miche ikitokeza.
7. Ruhusu miche ipate hewa na mwanga wa jua.
8. Andaa mashimo ya kupanda miche.
9. Weka mbolea kwenye mashimo na mwagilia maji.
10. Panda miche kwenye mashimo yaliyoandaliwa.



FOR ONLINE USE ONLY



Afya na Mazingira STD 2 _ 22 June 2021.indd 44 7/23/21 4:09 PM

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

11. Endelea kumwagilia mpaka miche ikue.



## Maswali

**Jibu maswali haya.**

12. Kwa nini tunafunika kitalu baada ya kusia mbegu?
13. Zipo mbegu zinazopandwa moja kwa moja kwenye mashimo. Taja majina matano ya mbegu hizo.
14. Kwa nini tunamwagilia miche?

## Kazi ya kufanya

1. Sia mbegu kwenye kitalu kilichoandaliwa.
2. Otesha mche mmoja shuleni kwa kufuata hatua. Vilevile, otesha mche mwingine nyumbani kwa kufuata hatua.
3. Mwagilia miche kila siku hadi ikue.
4. Andika kwa kifupi ulichojifunza tangu umeotesha mti hadi umekua kwa kuonesha changamoto na mafanikio.

FOR ONLINE USE ONLY




Afya na Mazingira STD 2 _ 22 June 2021.indd 45 7/23/21 4:09 PM

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE


## Tabia hatarishi katika mazingira

*Angalia picha zifuatazo, kisha jibu maswali.*


1.



2.



3.



4.



5.



6.



### Maswali

1. Taja tabia hatarishi zilizooneshwa kwenye picha.
2. Taja tabia ambazo si hatarishi katika picha hizo.



Afya na Mazingira STD 2 _ 22 June 2021.indd 46 7/23/21 4:09 PM

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Zoezi la 2

**Jibu maswali haya.**

1. Ukiogelea kwenye maji marefu utapata madhara gani?
2. Kati ya tabia zifuatazo zipi ni hatarishi?
   a) Kupanda juu ya miti mirefu.
   b) Kusaidia kazi za nyumbani.
   c) Kucheza sehemu zenye giza.
   d) Kufagia uwanja.
   e) Kuchezea wembe au kisu.
3. Andika tabia nyingine mbili hatarishi unazofahamu.


## Viumbe hatarishi katika mazingira

Vipo viumbe mbalimbali katika mazingira yetu. Viumbe hivyo ni kama vile nyoka, nyuki na mbu. Wengine ni tandu, simba, chatu, chui na fisi.

## Kazi ya kufanya


Kujigamba









FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE




## Zoezi la 3

**Jibu maswali haya.**

1. Orodhesha viumbe hatarishi nane unaowafahamu.
2. Taja viumbe hatarishi wanaopatikana katika mazingira ya nyumbani.
3. Kwa nini mbu ni kiumbe hatarishi kwa binadamu?
4. Taja viumbe hatarishi wanaopatikana porini.
5. Taja viumbe hatarishi wanaopatikana katika mazingira ya shule.

### Matumizi ya alama za tahadhari

Alama za tahadhari hutumika kuonya, kukataza na kuelekeza. Vilevile, hutambulisha hatari inayoweza kutokea

FOR ONLINE USE ONLY




Afya na Mazingira STD 2 _ 22 June 2021.indd 48 7/23/21 4:09 PM

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

endapo hutofuata maelekezo. Zifuatazo ni baadhi ya alama za tahadhari.


Alama ya moto


Alama ya umeme mkubwa


Alama ya hatari


Alama ya usafi wa mazingira


Alama ya kivuko cha waenda kwa miguu


Alama ya mlipuko


Alama ya hifadhi ya wanyama


Alama ya reli inakatisha


Alama ya taa za barabarani


Alama ya watembea kwa miguu


Alama ya njia ya waendesha baiskeli


Alama ya kivuko cha wanafunzi

FOR ONLINE USE ONLY




Afya na Mazingira STD 2 _ 22 June 2021.indd 49 7/23/21 4:09 PM

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Zoezi la 4

Tazama alama zifuatazo, andika maana ya kila alama

1.


2.


3.


4


**Jibu maswali haya.**

1. Taja alama za tahadhari zinazopatikana shuleni au nyumbani.
2. Ni alama gani za tahadhari zinazotumika barabarani?
3. Alama ifuatayo inakupa tahadhari gani?




FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

# Sura ya Nne

## Huduma ya kwanza



**Katika sura hii utajifunza vipengele hivi**

1. Kanuni za kutoa huduma ya kwanza.
2. Kutoa huduma ya kwanza.

FOR ONLINE USE ONLY




Afya na Mazingira STD 2 _ 22 June 2021.indd 51 7/23/21 4:09 PM

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Kanuni za kutoa huduma ya kwanza

Sanduku la huduma ya kwanza lina vifaa gani?



## Angalia picha hizi kisha jibu swali.





FOR ONLINE USE ONLY



Afya na Mazingira STD 2 _ 22 June 2021.indd 52
7/23/21 4:10 PM

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE






FOR ONLINE USE ONLY



Afya na Mazingira STD 2 _ 22 June 2021.indd 53 7/23/21 4:10 PM

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE






### Swali

Andika sentensi kutokana na picha katika matukio haya.

### Kazi ya kufanya

Kwa kushirikiana na wenzako fanya igizo kuonesha namna ya kutoa huduma ya kwanza.





Afya na Mazingira STD 2 _ 22 June 2021.indd 54 7/23/21 4:10 PM


FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE


# Kutoa huduma ya kwanza kwa mtu aliyenaswa na umeme

Angalia picha zifuatazo kisha fanya zoezi.








Afya na Mazingira STD 2 _ 22 June 2021.indd 55 7/23/21 4:10 PM

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Zoezi la 1

Tumia mtiririko wa picha kuandika sentensi nne.

## Kazi ya kufanya

Kwa kushirikiana na mwenzako igiza hatua za kutoa huduma ya kwanza.

### Maelezo ya Igizo

1. Igiza na wenzako kutoa huduma kwa mwenzenu. Mwenzenu ataigiza amepata ajali. Jeraha lioneshwe lina rangi nyekundu kama damu. Watoa huduma wawe na sanduku la huduma ya kwanza.

2. Toa huduma ya kwanza. Mwenzenu ataigiza kunaswa na umeme.

FOR ONLINE USE ONLY



Afya na Mazingira STD 2 _ 22 June 2021.indd 56 7/23/21 4:10 PM

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Kutoa huduma ya kwanza

Soma habari ifuatayo, kisha jibu maswali.

Shukuru na Tuli wanasoma shule ya Maarifa. Siku moja Tuli alimuuliza mama yake. Mbona hatuna sanduku la huduma ya kwanza? Mama yake akajibu, ukipata tatizo nitakupeleka hospitalini. Tuli alisikitika kutokana na lile jibu. Siku iliyofuata Shukuru alimpitia Tuli kwenda shule. Walipokuwa wanakaribia shuleni, Tuli alianguka akachubuka mguu. Shukuru alikimbia kutoa taarifa kwa mwalimu. Mwalimu na Shukuru walielekea alipoanguka Tuli. Shukuru alichukua sanduku la huduma ya kwanza. Shukuru alivaa glovu akasafisha michubuko. Alitumia pamba na spiriti ili kuua vijidudu.

Alipomaliza kumhudumia Tuli, alikusanya pamba na glovu. Alihifadhi vifaa hivyo sehemu husika. Vilevile alinawa mikono kwa maji safi na sabuni. Mwalimu na Shukuru walimpeleka Tuli zahanati kupata matibabu. Tuli aliporudi nyumbani alimsimulia mama yake yaliyompata. Mama yake alimpa pole. Mama yake aliwashukuru sana Mwalimu na Shukuru.

Aliona umuhimu wa sanduku la huduma ya kwanza. Hivyo Tuli alitengeneza sanduku la huduma ya kwanza. Mama yake alinunua sabuni, pini, wembe na spiriti. Aliongeza pamba, plasta, mkasi na bendeji. Tuli aliweka vifaa hivyo kwenye sanduku alilotengeneza. Tuli alifurahi sana.

FOR ONLINE USE ONLY



Afya na Mazingira STD 2 _ 22 June 2021.indd 57 7/23/21 4:10 PM

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Maswali

**Jibu maswali haya.**

1. Shukuru alivaa glovu kabla ya kumhudumia Tuli ili ________________.
2. Tuli alipata michubuko sehemu gani ya mwili?
3. Shukuru alibeba nini baada ya kutoa taarifa?
4. Tuli alipelekwa wapi baada ya huduma ya kwanza?

## Zoezi la 2

**Jibu maswali haya.**

1. Orodhesha vifaa vya sanduku la huduma ya kwanza.
2. Sanduku la huduma ya kwanza lina dawa mbalimbali. Taja dawa inayoua vijidudu.
3. Kwa nini ni hatari kuchezea nyaya za umeme?
4. Utafanya nini kumsaidia mtu aliyenaswa na umeme?
5. Taja vifaa vitano alivyonunua mama yake Tuli.

FOR ONLINE USE ONLY




Afya na Mazingira STD 2 _ 22 June 2021.indd 58 7/23/21 4:10 PM

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

# Sura ya Tano

## Viumbe hai katika mazingira











### Katika sura hii utajifunza vipengele hivi

1. Kutambua wanyama mbalimbali.
2. Kutambua mimea ya aina mbalimbali.




Afya na Mazingira STD 2 _ 22 June 2021.indd 59 7/23/21 4:10 PM


**Kutambua wanyama mbalimbali**




Paka




Mjusi




Chui




Chura



Mamba



Ng’ombe



Tembo


FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Kazi ya kufanya

Andika majina ya wanyama waliopo katika picha hizi.


1. 

4. 

2. 

5. 

3. 

6. 

FOR ONLINE USE ONLY



Afya na Mazingira STD 2 _ 22 June 2021.indd 61 7/23/21 4:10 PM

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Zoezi la 1

Angalia picha hizi, kisha jibu maswali.



1. Je, kuna wanyama wangapi katika ukurasa huu?
2. Taja wanyama wanaofugwa nyumbani.
3. Taja faida nne za kufuga wanyama hao.

FOR ONLINE USE ONLY



Afya na Mazingira STD 2 _ 22 June 2021.indd 62 7/23/21 4:10 PM

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

# Kutambua mimea ya aina mbalimbali




mpunga



alizeti



biringanya



mbuyu

FOR ONLINE USE ONLY



Afya na Mazingira STD 2 _ 22 June 2021.indd 63 7/23/21 4:10 PM

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE


## Kazi ya kufanya

1. Angalia picha, kisha andika jina la kila mmea.

1.




2.



3.



4.



2. Andika majina ya mimea mingine mitano unayoifahamu.



Afya na Mazingira STD 2 _ 22 June 2021.indd 64 7/23/21 4:10 PM

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Zoezi la 2

**Jibu maswali haya.**

1. Viumbe hai wapo katika makundi mangapi? Yataje.
2. Mimea ina faida gani?
3. Taja mimea inayopatikana kwenye mazingira ya shule yako.
4. Taja mimea minne inayotoa matunda.


FOR ONLINE USE ONLY





Afya na Mazingira STD 2 _ 22 June 2021.indd 65 7/23/21 4:10 PM


## Vitabu vingine kutoka
## Taasisi ya Elimu Tanzania


## Darasa la Kwanza



















## Darasa la Pili














## Darasa la Tatu















ISBN 978-9987-09-314-4

*Mali ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Hakiuzwi*